# HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI MHESHIMIWA PETER SIMON MSIGWA KUHUSU BAJETI YA WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

**(Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2016)**

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** hii ni hotuba yangu ya pili nikiwa Waziri Kivuli wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Leo tunajadili bajeti ya mwaka wa fedha 2017/18 ya wizara hii, nikiwa sijaridhishwa hata kidogo na kiwango cha usikivu ulionyeshwa na Serikali hii katika kutekeleza masuala mengi ya msingi, ambayo kambi ya upinzani iliyashauri mwaka jana kwa nia njema kabisa ya kulinyanyua Taifa!

**Mheshimiwa Spika,** ili Taifa letu liweze kupiga hatua kubwa sana kimaendeleo, ni muhimu sana viongozi wa Serikali na wabunge wa Chama cha Mapinduzi (CCM) wakazingatia ushauri huu aliowahi kuutoa mwanazuoni wa Korea ya Kusini, Jim Yong Kim; alisema, nanukuu:

***"No matter how good you think you are; as a leader, my goodness, the people around you will have all kinds of ideas for how you can get better. So for me, the most fundamental thing about leadership is to have the humility to continue to get feedback and to try to get better - because your job is to try to help everybody else get better",*** mwisho wa kunukuu.

***"Haijalishi unajiona bora kiasi gani kama Kiongozi, Ndugu yangu, watu walio karibu nawe bado watakuwa na kila aina ya mawazo ya jinsi ya kukufanya uwe bora. Kwa hiyo, kwangu Mimi, jambo la msingi kabisa kuliko yote katika uongozi ni kuwa na ustahimilivu wa kuendelea kupokea maoni na kujaribu kuwa bora zaidi – kwasababu kazi yako ni kujaribu kumsaidia kila mtu awe na maisha bora"***

**Mheshimiwa Spika**, ufike wakati sasa tutoke kwenye ***"hangover"*** (mawenge) ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2015" ili tuweze kuunganisha fikra zetu kwa faida ya nchi yetu. Haki na upendo huinua Taifa. Tuna Tanzania ya kujenga na tuna vizazi vya kuturithi. Wakati wa kuendekeza ujuaji, ubaguzi, dharau na vijembe visivyo na msingi sasa ni kheri ukafikia kikomo.

**Mheshimiwa Spika**, bila kujali itikadi za vyama vyetu, namuomba sana Mwenyezi Mungu Baba Aliye Juu atujalie busara ya kusikilizana zaidi, kuheshimiana zaidi na kukubali kuunganisha fikra zetu kwa manufaa ya Taifa letu. Kama alivyotujalia pumzi hata tukaifikia siku hii ya leo, basi na atujalie pia baraka za kitaifa ili tuweze kuyaona machweo ya ndoto njema za Tanzania yetu.

**Mheshimiwa Spika,** nichukue fursa hii kuwashukuru watu wangu wa nguvu wa Jimbo la Iringa Mjini kwa kuendelea kuniamini na kunipa jeuri ya kufanya kila lililo jema kwaajili yao na Taifa letu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa uzito wa kipekee, namshukuru Kiongozi Mkuu wa Kambi ya Upinzani Bungeni, Mhe. Freeman Mbowe (Mb), Mheshimiwa Riziki Shahari (Mb)-Naibu Waziri Kivuli pamoja na wabunge wenzangu wote wa kambi nzima ya upinzani, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) na Umoja wa UKAWA, kwa imani kubwa wanayoendelea kuwa nayo kwangu na kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu nikiwa Waziri Kivuli wa Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika,** nimkumbuke Kissa Msigwa - Mama Mchungaji huyu, Mke na Rafiki yangu kipenzi. Ndiye aliye nyuma ya mbwembwe zangu, ari na kasi kubwa niliyonayo katika kuutumikia umma wa Wana-Iringa na Watanzania wote bila kuchoka. Namshukuru sana Mama huyu na watoto wangu wote kwa kuendelea kuwa nami bega kwa bega bila kujali muda mwingi wanaonikosa nyumbani.

**Mheshimiwa Spika**, ni imani yangu kuwa hotuba hii imebeba maono na mwelekeo mpya juu ya namna bora zaidi ya kutimiza dira na dhima ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki, kwa maendeleo ya haraka ya Taifa letu.

**Mheshimiwa Spika,** Kauli mbiu ya hotuba hii ni ***Tufikiri Tofauti, Tupange Tofauti na Tutende Tofauti; Tanzania ya Tofauti inakuja.*** Ni imani yangu kuwa nitapewa usikivu wa kutosha kutoka kwa Bunge lako tukufu.

## 2.0 TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA SERA YA DIPLOMASIA YA UCHUMI

**Mheshimiwa Spika,** nianze na dira kuu ya sera mpya ya mambo ya nje: "***Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki, kwa mujibu wa dira hii, ndiyo inayopaswa kuwa mshawishi mkuu wa maslahi ya kiuchumi na maslahi mengine ya Tanzania kupitia ushirikiano na utengamano wetu na nchi, makampuni, taasisi na jumuiya mbalimbali za kimataifa na kikanda"***

**Mheshimiwa Spika,** ili kuifikia dira hii wizara inapaswa, pamoja na mambo mengine, kutumia mikakati ya diplomasia ya uchumi katika kuvutia fursa za kiuchumi kwa maslahi ya nchi yetu. Kama nilivyosema katika hotuba yangu ya mwaka jana, hizi ni zama mpya. ***Kama diplomasia ya kizamani ililenga zaidi kutafuta ukombozi, kulinda uhuru, mamlaka na amani ya nchi, basi diplomasia ya uchumi inalenga zaidi ustawi.***

**Mheshimiwa Spika,** diplomasia ya uchumi, pamoja na mambo mengine, inahusu kuvutia fursa za uwekezaji wa kigeni (foreign investments), utalii (tourism) na biashara huria (free trade) kwa kufanya ushawishi wenye kufungua masoko mapya ya kuuzia bidhaa za Kitanzania; kupunguza au kuondoa masharti ya kikodi; na kusaidia wafanyabiashara na wawekezaji wa Kitanzania kuzitumia kikamilifu fursa za kiuchumi zinazopatikana.

**Mheshimiwa Spika,** wakati hotuba yangu ya mwaka jana ilizungumzia jinsi Serikali ya CCM ilivyoshindwa kabisa kutekeleza sera ya diplomasia ya uchumi kwa zaidi ya miaka 15 iliyopita; mwaka mmoja wa Serikali ya awamu tano madarakani nao uliendelea kudumisha udhaifu ule ule wa Serikali za CCM ambao umekuwepo siku zote. Hakuna jitihada zozote za msingi zilizofanyika ili kujenga uwezo na ushawishi wa Serikali katika diplomasia ya uchumi.

**Mheshimiwa Spika,** utafiti uliofanywa na kambi ya upinzani hivi karibuni umebaini kuwa kuna sababu kuu mbili zinazoifanya Serikali ya Tanzania ifanye vibaya kwenye diplomasia ya uchumi:

**Mheshimiwa Spika,** kwanza, ukiondoa sera ya mambo ya nje inayotoa tamko la jumla tu kwamba ***"diplomasia ya uchumi ndio kipaumbele kikuu cha sera ya mambo ya nje***"; Tanzania haina ajenda ya taifa juu ya diplomasia ya uchumi wala mipango mikakati inayopimika (strategic plans) ambayo ingebeba vipaumbele mahsusi (specific priorities) juu ya nini hasa tunakitafuta kwenye kila taifa tunaloshirikiana nalo kwa maslahi yetu ya kiuchumi.

**Mheshimiwa Spika,** ili tuendelee ni lazima Serikali hii ikubali kufikiri tofauti, kupanga tofauti na kutenda tofauti. Ni lazima Serikali hii ikubali kusikia na kujifunza kutoka kwenye ***"akili kubwa"*** – kutoka Kambi Rasmi ya Upinzani na kutoka kwenye mataifa yaliyofanikiwa sana kwenye medani za kimataifa. Leo nawapeleka kidogo Australia!

**Mheshimiwa Spika,** Australia ni moja ya mataifa yenye uchumi mkubwa sana duniani. Sababu kuu ya kufanikiwa kwa taifa hili ni kutekeleza kwa umahiri na weledi mkubwa diplomasia ya uchumi. Mathalan, hadi kufikia mwishoni mwa mwaka jana (2016) thamani ya biashara ya nje ambayo Australia inafanya na nchi mbalimbali duniani ilikuwa ni sawa na asilimia 41 ya pato lote la taifa (GDP) la taifa hilo; na hii ni takwimu ambayo haijawahi kuporomoka tangu mwaka 1,900.

**Mheshimiwa Spika,** akizungumzia mafanikio ya nchi yake kwenye diplomasia ya uchumi, Mwanadiplomasia mahiri na waziri wa 38 wa Australia – Julie Bishop – alisema kuwa nchi yake imefanikiwa katika diplomasia ya uchumi kwasababu ya kuwa na mipango mikakati inayotekelezeka na yenye malengo na vipaumbele mahsusi juu ya diplomasia gani ifanyike kwenye kila nchi kati ya nchi zote 95 zenye ubalozi wa Australia duniani. Mpango mkakati wa kila ubalozi unatoa muongozo wa jinsi gani wanadiplomasia wa Australia watachochea ushirikiano wa kibiashara, kiuchumi na kiuwekezaji kwa niaba ya taifa lao kwenye nchi walizopo**.**

**Mheshimiwa Spika,** mbali ya Australia, jirani zetu wa Kenya nao wana mipango mikakati iliyo bora ya kutekeleza diplomasia ya uchumi kwenye balozi zao. Mfano mzuri ni mpango mkakati wa ubalozi wa Kenya mjini Cairo Misri ambao umeainisha vipaumbele mahsusi na kueleza kinaga-ubaga nini hasa Kenya inalenga kukipata kwa ushirikiano

wake na Misri. Hapa ndipo udhaifu wa kwanza wa Tanzania ulipo. Serikali ya CCM haina mipango bora inayoweza kutekelezeka na kupimika.

**Mheshimiwa Spika**, sababu ya pili ya nchi yetu kutopata mafanikio ya kuridhisha ni uhaba wa wanadiplomasia wenye weledi na umahiri kwenye diplomasia ya uchumi. Hatua ya Serikali kuteua mabalozi wa nchi za nje kwa kuzingatia zaidi u-CCM wao badala ya utalaam, uzoefu na umahiri wao kwenye diplomasia ya uchumi itaendelea kuikwamisha nchi kwa miaka mingi zaidi ikiwa Serikali haitabadilika.

**Mheshimiwa Spika,** mwaka jana Kambi ya Upinzani tulieleza jinsi Wizara ilivyoshindwa kwa muda mrefu kutoa mafunzo ya diplomasia ya uchumi kwa idadi ya kutosha ya maofisa wake. Tulisema, wakati Tanzania ikiwa na ofisi za ubalozi kwenye nchi 35 duniani, hadi kufikia mwezi Mei mwaka 2015 ni watumishi 32 tu ndio waliokuwa wamehitimu mafunzo ya muda mfupi ya diplomasia ya uchumi.

**Mheshimiwa Spika,** cha kusikitisha zaidi ni kuwa hata baada ya kambi ya upinzani kueleza mapungufu hayo, bado wizara haikuchukua hatua madhubuti za kumaliza tatizo hili. Sehemu ya Taarifa ya Wizara iliyowasilishwa kwenye Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama Januari 17 mwaka huu, pamoja na mambo mengine, ilisema, nanukuu:

“***Wizara imejiwekea mikakati mbalimbali katika kuhakikisha inatekeleza ipasavyo diplomasia ya uchumi. Mikakati hiyo ni pamoja na kuendelea kutafuta fursa mbalimbali za mafunzo ya diplomasia ya uchumi kwa watumishi wa wizara katika nchi marafiki; kutafuta fursa za ufadhili wa masomo za muda mfupi na muda mrefu kutoka nchi mbalimbali; kushirikisha maafisa katika makongamano na mikutano mbalimbali ya biashara na uwekezaji ili kuwajengea uwezo.”*** mwisho wa kunukuu.

**Mheshimiwa Spika,** taarifa hiyo ya Wizara inathibitisha jinsi Serikali isivyokuwa na umakini na inavyofanya mzaha na diplomasia ya uchumi, hasa ukitilia maanani ufafanuzi ufuatao;

- Maelezo ya Wizara yanathibitisha kuwa seriakali haijajipanga kabisa kufundisha watumishi yake yenyewe na badala yake inategemea kuokoteza fursa za kupeleka watumishi wake wakafundishwe diplomasia ya uchumi kwenye nchi rafiki kwa kadri zitakavyopatikana.
- Yanathibitisha kuwa Wizara haioni hata umuhimu wa kupanga bajeti ya kugharamia mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi ya diplomasia ya uchumi na badala yake itatafuta ufadhili. Kama ufadhili usipopatikana basi nchi itaendelea kupoteza fursa nyingi za kiuchumi zilizopo duniani kwasababu tu ya kuchelewa kuwa na wataalam wenye ujuzi wa diplomasia ya uchumi.

- Maelezo hayo ya wizara yanathibitisha kuwa kumbe Wizara inafanya ***"mzaha kazini"*** maana hupeleka watumishi mbumbu kwenye makongamano na mikutano nyeti ya biashara na uwekezaji ili tu wakajifunze nini maana ya diplomasia ya uchumi, wakati mataifa mengine hupeleka wanadiplomasia wake waliobobea ambao sio tu hunadi maslahi ya kiuchumi ya nchi zao bali pia ndio na hujenga msingi wa kuvutia fursa za kiuwekezaji na kibiashara kwa nchi zao.

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla maelezo hayo, wizara nzima inatia shaka juu ya weledi ilionao kwenye diplomasia ya uchumi. Ni hatari kutegemea elimu ya nje pekee katika kuwapa mafunzo watumishi wa wizara wakati ajenda za nchi ni tofauti; mafunzo makini juu ya diplomasia ya uchumi huenda sanjari na kufundisha ajenda mahsusi ya nchi husika.

## 3.0 MIRADI ILIYOTOKANA NA DIPLOMASIA YA UCHUMI

**Mheshimiwa Spika,** wizara imedai kupata mafanikio makubwa katika utekelezaji wa sera ya diplomasia ya uchumi. Taarifa iliyowasilishwa kwenye Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, tarehe 17 Januari 2017, imeyataja mafanikio hayo kuwa ni kuishawishi Serikali ya Uganda kupitisha Bomba la Mafuta kutoka Hoima, Uganda hadi bandari ya Tanga; na kuishawishi Benki ya Exim ya China kuwa tayari kutoa mkopo wa kujenga Reli ya Kati

kwa kiwango cha kimataifa (standard gauge). Pamoja na taarifa hiyo ya Wizara, baadae zilitolewa taarifa kuwa Serikali imepata mkopo wa ujenzi wa reli hiyo kutoka Uturuki na sio tena kutoka Benki ya Exim ya China, aidha kwa maneno ya Mkuu wa nchi ni kuwa fedha za ujenzi wa reli kwa kiwango cha standard gauge ni fedha zetu za ndani.

**Mheshimiwa Spika,** kambi ya upinzani haina tatizo na mafanikio haya na mengineyo yaliyoelezwa na wizara pamoja na taarifa za kukinza kuhusu fedha zitakazogharamia ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa. Kimsingi, huwa tunafarijika kila tunapoona jambo jema linatokea ndani ya nchi yetu. Hata hivyo, ni ukweli ulio dhahiri kuwa mafanikio yaliyoelezwa, bado ni finyu mno ikilinganishwa na fursa nyingi za kiuwekezaji, kitalii na kibiashara ambazo Tanzania inazo kulingana na jiografia yake, raslimali na mahitaji ya watu wake.

**Mheshimiwa Spika, 'diplomasia ya uchumi iliyofanikiwa ni ile inayojibu mahitaji ya ndani ya nchi husika'**. Wakati Tanzania ikiwa na ardhi kubwa inayofaa kwa kilimo, ikiwa ni pamoja na eneo kubwa linalofaa kwa kilimo cha umwagiliaji; na wakati zaidi ya asilimia 75 ya Watanzania wakiwa wamejiajiri kwenye kilimo duni cha jembe la mkono kisichotumia teknolojia wala mbinu za kisasa…bado mpaka sasa hakuna uwekezaji mkubwa uliofanyika kwenye sekta ya kilimo!

**Mheshimiwa Spika,** Tanzania ni nchi ya kilimo. Na sekta hii ndiyo inayoweza kuajiri Watanzania wengi na kuchangia sehemu kubwa ya pato la taifa (GDP). Kwa namna yoyote ile mafanikio ya Serikali katika diplomasia ya uchumi yalipaswa yaonekane kwanza kwenye kuvutia uwekezaji na biashara kwenye sekta hii pengine kuliko sekta nyingine yoyote ile.

**Mheshimiwa Spika,** wakati Serikali ikijinasibu kujenga "uchumi wa viwanda", bado sehemu kubwa ya nchi haina viwanda vya kuchakata na kusindika mazao ya kilimo na mifugo (***Agro-processing industries***). Sababu kuu ni ukosefu wa mitaji, teknolojia, na miundombinu. Hata hivyo, mahitaji yote haya ya kusukuma uchumi wa viwanda yangeweza kupatikana ndani na nje ya mipaka ya nchi kama Serikali ingeweza kutekeleza kwa ufanisi sera ya diplomasia ya uchumi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwingine, tathmini yetu inaonyesha kuwa yale ambayo wizara imekuwa ikidai kuwa ni ***mafanikio ya juhudi zake za kutekeleza sera ya mambo ya nje na diplomasia ya uchumi"***, kumbe wakati mwingine huwa ni juhudi binafsi tu za nchi za nje au makampuni ya kimataifa ambayo hujileta yenyewe kwa msukumo wa maono (***vision***) na ajenda zao za kimaendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mfano, taarifa za Kituo cha Uwekezaji (TIC) zinaonyesha kuwa mwitikio wa miaka ya hivi karibuni wa makampuni ya nje kuja kuwekeza nchini

umechagizwa zaidi na sekta ya madini na ugunduzi wa gesi. Hali hii inaashiria kuwa ukiondoa vivutio vya gesi, madini na uwindaji wa kitalii kwa kiasi fulani, ambavyo vimekuwa vikiwavuta wawekezaji moja kwa moja, bado Serikali imekuwa haina ajenda wala umahiri wowote wa kuvutia uwekezaji kwenye sekta nyingine zisizo na mvuto wa moja kwa moja kwa wawekezaji.

**Mheshimiwa Spika,** hii ndiyo siri ya Serikali kushindwa kuvutia uwekezaji wa kuridhisha kwenye sekta kilimo na ya viwanda vya kusindika na kuchakata mazao ya kilimo na mifugo (***agro-processing indurstries***). Uwezo wa wizara kutekeleza mikakati ya diplomasia ya uchumi umeishia kwenye kusubiria fursa zitufuate tu kuliko kuzitafuta.

**Mheshimiwa Spika, economic diplomacy is more of soliciting economic opportunities with your country's agenda than just waiting for foreign counterparts to advance their agenda through you!** Kwamba, diplomasia ya uchumi inahusu zaidi kufukuzia fursa za kiuchumi ukiongozwa na ajenda ya nchi yako kuliko kusubiria tu nchi rafiki zikufuate zikiwa na ajenda zao.

**Mheshimiwa Spika,** uzoefu unaonyesha kuwa nchi zote zilizofanikiwa kwenye diplomasia ya uchumi duniani kama Australia na India ni zile zilizojituma kufukuzia fursa kwenye nchi nyingine, zikiongozwa na ajenda mahsusi kwa maslahi ya raia wao. Si jambo la kujivunia hata kidogo kumuona Mwanadiplomasia wetu namba moja (Rais) akifanya kazi

ya kupokea viongozi wakuu wa nchi nyingine tu huku Serikali yetu ikiwa haijitumi vya kutosha kufukuzia fursa kwenye mataifa mengine.

## 4.0 MAPENDEKEZO YA KUONGEZA UFANISI KWENYE UTEKELEZAJI WA SERA YA MAMBO YA NJE

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji makini wa sera ya mambo ya nje hususan diplomasia ya uchumi, unaweza kuleta tija kubwa katika kuharakisha ukuaji wa uchumi na maendeleo ya nchi. Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliwahi kusema: **"Kwa jinsi tulivyoachwa nyuma, Watanzania tunapaswa kukimbia wakati wenzetu wakiwa wanatembea".** Wakati mataifa makubwa duniani, kama Australia, Marekani, China na hata India, yakizidi kupiga hatua kubwa za kimaendeleo kwa kujiimarisha kwenye diplomasia ya uchumi; Tanzania yetu maskini lakini yenye fursa kubwa za utajiri, haina budi kuchukua hatua madhubuti na za haraka za kutekeleza diplomasia ya uchumi kwa weledi na umahiri wa hali ya juu.

**Mheshimiwa Spika,** ili kuboresha utekelezaji wa diplomasia ya uchumi na sera ya mambo ya nje kwa ujumla, Kambi ya Upinzani kwa kujali maslahi ya mapana ya Tanzania yetu, inaishauri Serikali ifanye yafuatayo;

**Mheshimiwa Spika**, kwanza, Serikali itengeneze Agenda ya Diplomasia ya Uchumi ya Tanzania yenye kuanisha malengo na vipaumbele vinavyopimika. Hapa Kambi ya Upinzani inashauri zaidi kuwa sekta ya kilimo, nishati ya

umeme vijijini na ile ya viwanda vya kuchakata mazao ya kilimo na mifugo (Agro-processing indurstries), ndizo zipewe kipaumbele kikubwa katika kuvutia uwekezaji wa moja kwa moja kwa mitaji ya nje (direct foreign investments) na teknolojia kwa maendeleo ya sekta hizi.

**Mheshimiwa Spika,** Agenda ya Diplomasia ya Uchumi ya Tanzania isijikite tu kwenye balozi, bali pia ibebe masuala ya kipaumbele ya kufanyiwa kazi kidiplomasia hadi kwenye jumuiya za kikanda, ikiwemo jumuiya ya Afrika ya Mashariki (EAC). Hapa umuhimu wa pendekezo hili unazidi kuwa mkubwa hasa ikizingatiwa kuwa Tanzania imekuwa ikishiriki kwenye EAC, SADC na jumuiya nyingine za kikanda bila hata kuwa na sera ya utengamano.

**Mheshimiwa Spika,** pili, wizara ihakikishe kuwa ubalozi wa Tanzania kwenye zote 35 duniani unakuwa na mpango mkakati wa diplomasia ya uchumi ***(strategic plan)*** uliojikita kwenye matokeo ***(result-based)*** na unaoweza kutekelezeka na kupimika ndani ya vipindi vifupi na vipindi virefu vya utekelezaji.

**Mheshimiwa Spika,** tatu, mipango mikakati ya kila ubalozi iunganishwe na kuwa na mpango kabambe mmoja wa Wizara. Huu ujikite zaidi kwenye kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa diplomasia ya uchumi kwa balozi zote na nchi nzima kwa ujumla. Pamoja na mambo mengine mpango huu wa wizara uweke malengo ya muda mrefu na ya muda mfupi ya kuandaa wanadiplomasia waliobobea kwenye fani ya diplomasia ya uchumi.

**Mheshimiwa Spika,** tatu, wizara ikishirikiana na Kituo cha Uwekezaji (TIC) ifanye mapitio upya juu ya uhalisia wa lengo la kuongeza uwekezaji wa moja kwa moja wa kigeni "foreign direct investment (FDI)" nchini kutoka Dola za Kimarekani Bilioni 1.5 kwa mwaka 2015 hadi kufikia Dola za Kimarekani Bilioni 5, ifikapo mwaka 2020. Utafiti wa kambi ya upinzani umebaini kuwa lengo lililowekwa na TIC ni dogo sana ikilinganishwa na fursa kubwa zilizopo za Tanzania kupata FDI kubwa zaidi kama Serikali itaacha mzaha kwenye kutekeleza diplomasia ya uchumi.

**Mheshimiwa Spika,** upo msemo usemao ***"mafanikio ni kama bahari, tatizo letu baadhi tunapokwenda kuyachota huwa tunakwenda na vijiko".*** Lengo dogo la kufikia FDI ya Dola Bilioni 5 mwaka 2020 linaweza kabisa likaifanya Tanzania kuendelea kufanya jitihada ndogo kwenye diplomasia ya uchumi. Aidha, lengo hilo dogo la TIC lipo mbali sana na ndoto ya Tanzania ya kutaka kuwa nchi yenye uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025, kwani nchi zote zilizo kwenye uchumi wa kati zina sifa ya kupata FDI kubwa.

**Mheshimiwa Spika,** ni vema ikakumbukwa kuwa Tanzania mwaka 2014, nchi yetu ilishapokea jumla ya uwekezaji wa mitaji ya moja kwa moja ya kigeni (FDI) ya thamani ya Dola Bilioni 2 za Kimarekani. Hii inaashiria kuwa Tanzania inaweza kabisa kupata zaidi ya Dola Bilioni 5 za Kimarekani ifikapo mwaka 2020.

## 5.0 USHIRIKIANO NA UKUZAJI WA MAHUSIANO YA KIDIPLOMASIA NA MATAIFA MENGINE

**Mheshimiwa Spika,** nchi yetu ilijijengea heshima kubwa katika medani za kimataifa hasa kwenye masuala ya kupigania uhuru wa nchi nyingine barani Afrika, pamoja na kutetea nchi ambazo zilikuwa zinaonewa na mataifa mengine duniani.

**Mheshimiwa Spika,** Ushirikiano wa kimataifa kwa nchi inayoendelea kama Tanzania ni jambo la msingi sana kwani kuna mambo mengi ambayo tunahitaji kujifunza kutoka kwa mataifa mengine ili kuweza kuasili mabadiliko ya kisayansi, kiteknolojia, kiuchumi na kiutandawazi yanayoendelea kutokea kila siku duniani.

**Mheshimiwa Spika,**wakatia akiwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani katika bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Kiongozi wa Upinzani Bungeni Mheshimiwa Freeman Mbowe (Mb) alisema kwamba; Licha ya umuhimu wa kuwa na ushirikiano wa kidiplomasia na mataifa mengine;Serikali ya awamu ya tano imeonekana kwenda na dhana hiyo kwa kudhibiti safari za nje kwa kisingizio cha kubana matumizi. Aliitahadharisha Serikali kwamba; kudhibiti safari za nje ni kuliingiza taifa kwenye giza nene kwani safari hizo zilikuwa ni lango la fursa za biashara ya kimatafa (international trade) ambayo ndiyo msingi wa diplomasia ya ki-uchumi.

**Mheshimiwa Spika,** ushirikiano wa kimataifa unaimarishwa pale ambapo wakuu wa nchi mbalimbali wanapokutana kujadili masuala mbalimbali kuhusu mustakabali wa nchi zao na namna ya kusaidiana kukabiliana na changamoto mbalimbali. Ni jambo la kustaajabisha kuona Rais wa nchi

yetu akiwa na mwamko mdogo wa kushiriki mikutano ya kimataifa kwa ajili ya kukuza ushirikano na mataifa mengine. Kitendo cha Rais kushindwa kuhudhuria Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN General Assembly) mwaka jana kimeiweka Tanzania nyuma katika uhusiano wa kimataifa.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na kutambua kuwa Rais amekuwa akituma wawakilishi katika mikutano ya kimataifa, lakini vipo vikao au mikutano ya kimkakati (strategic meetings) ambayo ni lazima Rais wa nchi kushiriki.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatoa rai kwa Rais kuacha kukwepa kuhudhuria mikutano ya kimataifa na ya kikanda ambayo ni muhimu kwa ajili ya kujenga mustakabali wa diplomasia ya uchumi pamoja na uhusiano wa kimataifa kwa ujumla kama ambavyo umekuwa ni utamaduni wa taifa letu. Aidha, washauri wa Rais hasa wa masuala ya kimataifa wamshauri Rais juu ya umuhimu wa ushiriki wake katika vikao na mikutano hiyo pamoja na kuzingatia itifaki za kimataifa.

**Mheshimiwa Spika,** kuna udhaifu mkubwa sana katika Serikali hii wa kutozingatia itifaki za kimataifa. Haingii akilini Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa anakuja nchini halafu anapokelewa na Waziri wa Mambo ya nje wakati Rais yupo; lakini wakati huo huo Rais anafanya kikao na Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama cha Kikomunisti cha China. Inaweza kuonekana kama ni kawaida tu Rais kutompokea Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa; na inaweza kuonekana

jambo la kawaida pia Rais kufanya kikao na Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama cha Kikomunisti cha China lakini katika jicho la kidiplomasia kuna makosa makubwa sana ya kiitifaki yanayofanywa na Ofisi ya Rais.

**Mheshimiwa Spika,**uhusiano wa kimataifa unaweza kuathiriwa na namna sisi kama taifa tunavyowatendea raia wa nchi nyingine wanaoishi au kufanya kazi katika nchi yetu. Mataifa mengine huwa yanajali sana hali za raia wao wanaoishi au kufanya kazi katika mataifa mengine. Hivyo, mataifa hayo huwa yako tayari hata kupigana vita kwa ajili ya raia wao wanaonyanyaswa au kutendewa visivyo katika nchi nyingine.

**Mheshimiwa Spika,** kitendo cha hivi karibuni cha Rais wetu kuagiza pasi ya kusafiria ya mkandarasi kutoka India ambaye anajenga mradi wa maji wa Ngapa huko Lindi kutokana na makosa aliyoyafanya katika mradi huo unaweza kuingiza nchi yetu katika mgogoro wa kidiplomasia kwa sababu pasi ya kusafiria ni mali ya taifa ambalo limetoa pasi hiyo. Na katika pasi hiyo kuna tamko la Rais wa nchi husika linaloomba raia huyo apewe ulinzi na msaada wowote atakaohitaji katika nchi atakayokuwa ameingia kuishi au kufanya kazi.

**Mheshimiwa Spika,** ikumbukwe kuwa utamaduni duniani ni kuwa; pasi ya kusafiria hutolewa na Rais wa nchi husika kwenda kwa mamlaka ya nchi ambayo mtu anasafiri kwa ajili kupata msaada wowote anaohitaji kulingana na malengo ya safari yake na taratibu za nchi aliyopo. Hata

Sheria yetu inayosimamia utoaji wa pasi na nyaraka nyingine za kusafiri kifungu cha nne kinatamka kuwa pasi inatolewa na Rais kwa ajili ya kumtambulisha Mtanzania katika mamlaka ya nchi nyingine na kupatiwa msaada na usaidizi wowote atakaohitaji kwa mujibu wa taratibu za nchi husika. Hivyo, kuagiza pasi hiyo kushikiliwa ni kuidhalilisha mamlaka iliyotoa pasi hiyo kwa maana ya Rais wa nchi husika jambo ambalo linaiingiza nchi yetu katika mgogoro wa kidiplomasia moja kwa moja.

**Mheshimiwa Spika,** agizo la Rais la kushikilia *passport* ya mkandarasi huyo tayari limeripotiwa katika vyombo mbalimbali vya habari vya kimataifa ambavyo kwa vyovyote vile vinasomwa na watu mbalimbali duniani wakiwemo wawekezaji.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali ina vyombo vya ulinzi na usalama mpaka mipakani, kama mwekezaji au mkandarasi kutoka nje amepewa maelekezo ya kumaliza mradi kwa muda flani, ni vema akapewa nafasi ya kufanya hivyo bila kuchukua pasi yake ya kusafiria. Mambo yote hayo yanafanyika kwa mujibu wa mikataba ambayo Serikali imeingia na wawekezaji au wakandarasi na hivyo ni vema mikataba ikazingatiwa na au maelekezo/makubaliano mengine kuliko kuanza kuchukua pasi za kusafiria za mataifa mengine.

**Mheshimiwa Spika,** athari za maamuzi au amri za Rais zinaweza zisionekane leo lakini kwa utafiti wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ni kuwa agizo la Rais la kuamuru pasi

ya raia mwingine kuchukuliwa liliripotiwa katika vyombo vya habari vingi duniani pamoja na nchi ya India yenyewe. Jambo hili si tu linatia doa nchi yetu katika masuala ya uhusiano wa kimataifa lakini pia linaweza kuleta athari katika sekta ya uwekezaji.

## 6.0 MIRADI YA MAENDELEO YA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inatambua kuwa ipo miradi ya maendeleo ndani ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki ambayo hugharamiwa na washirika ndani ya Jumuiya pamoja na wadau mbalimbali duniani hasa Umoja wa Ulaya. *Gazeti la The Citizen* la tarehe 17 Mei 2017 ukurasa wa 15 liliripoti kuwa Jumuiya ya Afrika imekumbwa na tatizo ukosefu wa fedha za kukamilisha miradi ya maendeleo ambayo hugharamiwa na Jumuiya hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na kuwa suala la kuchangia miradi ya maendeleo lipo kwa mujibu mkataba unaoanzisha Jumuiya ya Afrika ya Mashariki bado michango ya kifedha za baadhi ya washirika ndani ya Jumuiya imekuwa haitolewi kwa ukamilifu ikiwemo nchi yetu. Ieleweke kuwa ibara ya 132(4) inaelekeza kuwa bajeti kwa ajili ya Jumuiya zitachangiwa kwa usawa na nchi washirika ndani ya Jumuiya.

**Mheshimiwa Spika**, imeonekana wazi kuwa nchi wanachama zinaanza kugawanyika kuhusu utaratibu wa kuchangia miradi ya maendeleo ambapo nchi kama Burundi inaona kuwa haiwezi kuchangia sawa na zingine

washirika kutokana na matatizo yake ya ndani. Hata hivyo baadhi ya nchi kama Tanzania imekuwa haitoi fedha za miradi ya maendeleo kwa wakati hivyo kuwa kikwazo katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Ikumbukwe kuwa 40% bajeti ya miradi ya maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki inagharamiwa na nchi washirika huku 60% ikigharamiwa na nchi washirika.

**Mheshimiwa Spika**, taarifa inaonesha kuwa kwenye bajeti ya miradi ya maendeleo ya Jumuiya ni takribani dola milioni 101.6 ambapo kila nchi hutakiwa kuchangia kiasi cha dola milioni 8.3. Takwimu zinaonesha kuwa hadi kufikia Machi mwaka huu ni nchi ya Kenya pekee ambayo imetoa mchango wake kwenye bajeti ya maendeleo kwa 100% ikifuatiwa na Uganda 90%, Rwanda 51%, Tanzania 35% na Burundi 0%.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani haijashangaa kuona Tanzani imetoa 35% ya bajeti ya miradi ya maendeleo katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa sababu hata kwenye miradi ya maendeleo ya ndanikatika Wizara mbalimbali Serikali haikuweka msisitizo kutoa fedha za miradi ya maendeleo, ndiyo maana baadhi ya Wizara bajeti ya miradi ya maendeleo imetolewa kwa kiasi kidogo, mathalani Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi katika sekta ya Kilimo ni 3% pekee fedha za maendeleo zilizokuwa zimetolewa hadi kufikia mwezi Mei 2017.

**Mheshimiwa Spika**, ieleweke kuwa miradi ya maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki inanufaisha pia nchi yetu kama

moja ya nchi washirika ndani ya Jumuiya. Tanzani imekuwa ikilalamikiwa na wadau wa jumuiya ya Afrika Mashariki kuwa moja ya nchi ambayo mara kadhaa imekuwa kikwazo cha maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa haiwi kikwazo kwa kazi mbalimbali za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki hasa kwenye miradi ya maendeleo. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge lako tukufu sababu za kutotoa fedha za maendeleo kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

## 7.0 UHUSIANO NA MAJIRANI ZETU

**Mheshimiwa Spika,** mahusiano na jirani ni kitu kikubwa Sana, na ndio maana kuna msemo unasema jirani yako ni zaidi ya ndugu yako na mara zote huwezi kuchagua jirani bali unachagua rafiki. Hivyo basi hata kama jirani yako sio wa chaguo lako ni lazima uishi nae vizuri tu na ndio utu , imani na utamaduni wetu wa asili.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani imeanza kwa kutoa bashrafu hiyo kutokana na taarifa zilizochapishwa kwenye gazeti linalotolewa kila siku nchini Kenya Daily Nation, toleo la tarehe 14 Mei, 2017 lilimnukuu Kiongozi wa wabunge katika Bunge la Kenya Mhe. Aden Duale akitoa shutuma kwamba Tanzania inapanga kuingilia mchakato wa uchaguzi wa nchi hiyo, kwa kuweka kituo cha majumuisho ya kura za Urais kwa jumuiko la vyama vya Upinzani nchini Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** shutuma hizi sio za kuzipuuzia kwa urahisi tu kwani zilitolewa ndani ya Bunge hilo la Kenya na hivyo zina athari za moja kwa moja katika masuala ya kidiplomasia ndani ya Jumuiya. Tumeshuhudia hivi karibuni Rais wa Kenya akishindwa kuhudhuria vikao vya Jumuiya mara kadhaa na kumtuma Naibu  Rais wan chi hiyo jambo ambalo linapelekea wananchi wengi kujiuliza ni nini hasa kinachomfanya Rais Kenyata kushindwa kuhudhuria vikao vinavyofanyika Tanzania kwa mara ya pili sasa?

**Mheshimiwa Spika,** tukirejea katika Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki Kifungu cha 6 (d), Kifungu cha 7 (2) ambapo vifungu hivi vinasisitiza misingi ya utawala bora unaozingatia misingi ya kidemokrasia, utawala wa sheria,uwazi na uwajibikaji n.k ambapo nchi wanachama wanatakiwa kufuata misingi hii. Endapo Tanzania tutaanza kuingilia chaguzi hizi basi tujue dhahiri tutakuwa miongoni mwa wachochezi wanaohatarisha amani za nchi za wenzetu. Kambi Rasmi ya Upinzani inalaani kabisa machafuko yale yaliyotokea nchini Kenya mwaka 2007 na kwa namna yoyote hatuwezi kuona hali ile ikijirudia

Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulizungumzia jambo hili kwani kuendelea kukaa kimya kuna maanisha kuwa Msemaji aliyetoa shutuma hizi ndani ya Bunge la Kenya ni za kweli.

## 8.0 MSIMAMO WA TANZANIA JUU YA MATUKIO MBALIMBALI DUNIANI

**Mheshimiwa Spika,**nchi yetu imekuwa na historia iliyotukuka duniani, ya kuwa mstari wa mbele kupinga  aina zote za uonevu, unyonyaji na utumwa hususan ubeberu na ukoloni. Kutokana na tunu yake ya kujali utu na usawa miongoni mwa binadamu wote,  Tanzania ya enzi za Mwalimu Nyerere, ilifikia hatua ya kujitoa kupigana vita vya ukombozi wa nchi za kusini mwa Afrika, ili kuhakikisha  kwamba ubeberu na ukoloni katika nchi hizo unatokomezwa na uhuru wa kweli unapatika.

**Mheshimiwa Spika,** itakumbuka kwamba Tanzania ndiyo iliyokuwa muasisi wa nchi za wa mstari wa mbele  chini ya uongozi wa Mwalimu Nyerere katika miaka ya 1960 kwa lengo la kupinga ubaguzi wa rangi na utawala wa wazungu wachache katika nchi za kusini mwa Afrika.

**Mheshimiwa Spika,**Tanzania ilienda mbele zaidi hadi  kufikia hatua ya kuvunja mahusiano yake ya  kidiplomasia na mataifa mengine yaliyokuwa na tabia za ubaguzi wa rangi, unyonyaji, ubeberu na ukoloni dhidi ya mataifa mengine. Tanzania ilipinga pia utawala wa kidikteta miongoni mwa nchi za Afrika, kwa kuwa udikteta ulikuwa na tabia zote za unyonyaji, ubaguzi, uonevu na ukiukwaji wa haki za binadamu ,mambo ambayo Watanzania hawakuamini katika hayo na ndio maana Tanzania kwa  wakati huo, haikumuunga mkono Mobutu Seseko wa iliyokuwa Zaire – sasa Kongo DRC, haikumuunga mkono Muamar Gadafi wa Libya na pia ilimng'oa madarakani dikteta wa Uganda Idd Amin Dadah.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua kuwa Tanzania bado inatekeleza sera na msimamo wake wa kidiplomasia wa kutofungamana na upande wowote kwenye migogoro ya kiitikadi na misimamo kadhaa ya mataifa mbalimbali duniani..

## 7.1 Msimamo wa Tanzani kuhusu Morocco na Mataifa Mengine

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 23 Oktoba, 2016 nchi yetu ilipokea ugeni kutoka Morocco ambapo mfalme wa nchi hiyo akiambatana na watu takribani 150 alitutembelea. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua kuwa Morocco sio sehemu ya Umoja wa Afrika kwa sasa kutokana na mgogoro wake na Sahara ya Magharibi.

**Mheshimiwa Spika**, 1971 vuguvugu la POLISARIO lilianzishwa na wanafunzi wa vyuo vikuu wenye asili ya watu wa Sahrawi ambao ni jamii ya watu wanaoishi Sahara Magharibi waliokuwa wanapigania uhuru wa Jimbo lao kuwa nchi. Baadae Sahara Magharibi ikatambuliwa na Umoja wa Mataifa huku nchi ya Morocco ikipinga na ikiendelea kuikalia sehemu hiyo kimabavu hadi leo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa taarifa zilizotolewa na Waziri wa Mambo ya Nje na kunukuliwa na vyombo vya habari nchini ni kuwa pamoja na uhusiano wa Tanzania na Morocco bado kama taifa hatujayumba kwenye msimamo wetu wa kuitaka Morocco kuiacha huru Sahara Magharibi kwa sababu zama za ukoloni zimeshapitwa na wakati. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kuwa Serikali inayumba

kwenye msimamo wake dhidi ya Morocco kwa sababu mazingira ya miaka ya 1970 ni yale yale ambapo mpaka sasa Morocco bado inaikalia kimabavu Saharra Magharibi.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kuwa uhusiano wa Morocco na Tanzania ni mwendelezo wa Morocco kutaka kurudi kuwa mwanachama wa Umoja wa Afrika huku ikiendelea kuikalia Sahara Magharibi. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge lako tukufu undani wa uhusiano wa Tanzania na Morocco na taarifa ya kina ya makubaliano yaliyofikiwa kati ya nchi hizo mbili. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa kwa sasa nchi yetu inayumba kwenye diplomasia kwa sababu imeshindwa kuwatetea wanyonge wa Sahara Magharibi huku ikiikumbatia Morocco. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaikumbusha Serikali kuwa tarehe 03 Mei, 1967 Jimbo la Biafra la nchini Nigeria lilitangaza kujitenga na Nigeria ya Kaskazini ambapo wananchi wa Jimbo hilo waliona kuwa ni vema wakajitenga na kuunda taifa lao kutokana na vifo na mateso waliyokuwa wanakumbana nayo.

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 13 Aprili, 1968 Tanzania ilikuwa nchi ya kwanza kulitambua Jimbo hilo kama nchi huru. Pamoja na mjadala mkali uliokuwepo wakati huo juu ya msimamo wa Serikali lakini angalau wakati Serikali ilikuwa na msimamo thabiti ya kutetea wanyonge. Ni rai ya Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni kwa Serikali kuhakikisha kuwa ile

misingi mizuri iliyokuwepo inaenziwa na sio kuyumba kulingana na maslahi ya sasa.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge lako tukufu juu ya msimamo wetu kama nchi kuhusu mgogoro uliopo Syria, Mgogoro kati ya India na Jimbo la Kashmiri, Mgogoro unaoashiria vita kati ya Marekani na washirika wake dhidi ya Koreah ya Kaskazini.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inatambua urafiki kati ya Chama cha Mapinduzi na Chama cha Kikomunisti cha China. Ieleweke kuwa mbali na Morocco, Taifa la China lipo kwenye mgogoro na Jimbo la Tibet na Taiwan kwa muda mrefu na China ikipewa lawama kuwa inazikalia sehemu hizo kimabavu. Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kuhoja msimamo wa Serikali kuhusu mgogoro wa China na sehemu hizo ambayo imekuwa ya muda mrefu.

### 7.2 Brexit na Umoja wa Ulaya

**Mheshimiwa Spika**, mwaka uliopita haukuwa mzuri kwa Umoja wa Ulaya baada ya Taifa kubwa la Uingereza ndani ya Umoja huo kuamua kujitoa katika Umoja huo kufuatia kura ya maoni ya wananchi wa nchi hiyo maarufu kama Brexit.

**Mheshimiwa Spika**, Sakata la Brexit kwa vyovyote vile litaathiri masuala ya diplomasia duniani kwa sababu bado Umoja wa Ulaya una uhusiano wa karibu na nyingi za kiafrika Tanzania ikiwemo. Aidha, baada ya kura ya maoni

na kuanza kupeleka rasmi maombi ya kujitoa katika Umoja wa Ulaya Taifa la Uingereza imeanza kwa kasi kujenga na kuboresha mahusiano ya kidiplomasia kati yake na mataifa mbalimbali duniani.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kufanya tathmini ya kina juu ya Brexit na Umoja wa Ulaya ili kuona ni wapi tutasimama kama nchi hasa kwenye masuala ya diplomasia ya uchumi kwa sababu kwa vyovyote sakata hilo litaathiri baadhi ya masuala ya kidiplomasia. Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua kuwa Tanzania imekataa kusaini mkataba wa EPA ambao unapigiwa chapuo na Umoja wa Ulaya na baadhi ya nchi washirika wa Afrika Mashariki.

**Mheshimiwa Spika,** msimamo wa Tanzania kutosaini mkataba wa EPA unaweza kuimarisha mahusiano ya kiuchumi na Taifa la Uingereza baada ya Brexit. Kambi Rasmi ya Upinzani inasisitiza kwa Serikali kufanya tathmini ya kina na kuweka msimamo wake kuhusu mahusiano haya ambayo yanaenda kuwa na mabadiliko makubwa.

## 8.0 UONEVU WANAOFANYIWA WATANZANIA NJE YA NCHI-WATANZANIA KUFUKUZWA MSUMBIJI

**Mheshimiwa Spika,** hivi karibuni kumeanza kushamiri kwa tabia ya baadhi ya nchi kuwafukuza wananchi wa nchi nyingine kwa kisingizio cha kunyang’anywa ajira za wazawa. Tanzania imekuwa miongoni mwa waathirika wakubwa katika kadhia hii. Kwa mujibu wa gazeti la

Mwananchi la tarehe 16 Februari 2016 ,watanzania wapatao 180 walifukuzwa nchini Msumbiji.

**Mheshimiwa Spika,** Watanzania hawa walipoteza mali, fedha, marafiki na waliathirika sana kiuchumi, kisaikoloji n.k. Watanzania hawa walitoa malalalamiko yao ambayo kwa sehemu kubwa yalilwaenga askari wa Msumbiji ambao walilalamikiwa kuwapora wakati wa operesheni hiyo ya kamatakamata. Wengine walilazimika kuacha wazi sehemu zao za biashara na kukimbia kwa kuhofia maisha yao. Watanzania waliokamatwa waliwekwa mahabusu bila kufuata taratibu za kisheria. Wengi walikaa mahabusu kwa siku kadhaa na kisha kupelekwa eneo la mpaka wa Kilambo mkoani Mtwara ambapo ni mpaka wa Tanzania na Msumbiji na kutelekezwa huko bila kujali utu wala mahusiano ya ujirani mwema ambao umetengenezwa na Waasisi wa Mataifa haya kwa miaka mingi.

**Mheshimiwa Spika,** mbali na madhila hayo yaliyowatokea Watanzania wenzetu; Mheshimiwa Rais alinukuliwa na vyombo mbalimbali vya habari mnamo tarehe 05 Machi 2017, akiwa kwenye ziara Mkoani Mtwara aliwataka wananchi hao kuacha kukuza suala la Watanzania waliofukuzwa nchini Msumbiji ambao aliwaita wahamiaji haramuna alisisitiza kuwa Serikali haiwezi kuwatetea watu waishio katika nchi nyingine bila kufuata sheria. Pamoja na hayo Mheshiwa waziri alitoa maelezo kuhusiana na kufukuzwa kwa Watanzania hao nchini Msumbiji na alieleza

kuwa madhila yaliyowapata Watanzania wenzetu yanaweza kuendelea ***(Operation fukuza watanzania***) kwani mji uliokumbwa na tukio hilo wa Monte Puez uliopo Jimbo la Cabo Delgado kuna idadi ya Watanzania wanaokadiriwa kuwa takribani 3000.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kufahamu yafuatayo:
Je, Mheshimiwa Rais alipewa habari za uhakika kuhusiana na Watanzania walofukuzwa nchini Msumbiji?Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inauliza swali hili kwa sababu wapo Watanzania waliofukuzwa na walikuwa na vibali halali za kufanya kazi nchini humo.
Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kujua ni nini hasa wajibu wa Balozi katika kusimamia usalama wa Watanzania na mali zao wanapokuwa nje ya nchi kwa majukumu mbalimbali hasa tukizingatia nchi yetu inajipambanua katika kusimamia sera mpya ya Diaspora kama ilivyo katika tovuti ya Wizara?

## 9.0 MAUAJI YA WATANZANIA NCHINI OMAN

Mheshimiwa Spika, siku za hivi karibuni kumekuwa na matukio ya unyanyasaji na mauaji ya watanzania wanaofanya kazi nje ya nchi hususani nchini Oman. Matukio mengi ya unyanyasaji yameripotiwa na vyombo mbalimbali vya habari na pia kwenye ngazi za familia za wahusika, lakini kutokana na hali ya umasikini wa familia

nyingi zilizokumbwa na madhila haya hakuna hatua zozote zilizochukuliwa dhidi ya wahusika ambao ni raia wa Oman.

**Mheshimiwa Spika,** mnamo tarehe 14 Machi, 2017 Msichana wa Kitanzania mkazi wa Dar es salaam ambaye alikuwa anafanya kazi za ndani mtaa wa Bilad Ban Bu Alli nchini Oman aliuawa kwa kutupwa toka ghorofani jambo lililompelekea umauti. Hili ni moja tu ya matukio ya ukatili na ya kutisha wanayofanyiwa Watanzania hasa wanawake wanaofanya kazi za majumbani nje ya nchi hususani katika nchi za Arabuni na India kama Kambi ya Upinzani Bungeni ilivyoelezea katika hotuba yake ya bajeti kupitia Wizara hii mwaka 2016/2017.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi inataka kufahamu ni kwanini mambo haya yamekuwa yakizungumziwa lakini Serikali haichukui hatua madhubuti? Ni kwa nini taarifa rasmi kuhusu mauaji ya Mtanzania huyu aliyeuawa kinyama haijatolewa na kulaaani matendo haya ya kinyama wanaofanyiwa Watanzania waishio Oman na maeneo mengine ?Je, Serikali ina mikakati gani ya kuwatambua mawakala wote wanaojihusisha na kuwatafutia kazi za ndani Watanzania huko ughaibuni ili matatizo yanapotokea iwe rahisi kuwabaini wahusika?

## 10.0 WATANZANIA WALIOFUNGWA NCHINI CHINA

**Mheshimiwa Spika,** Watanzania waliofungwa katika magereza mbali mbali Nchini China wanapata taabu na

mateso kinyume na haki za binadamu na mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Vienna wa mwaka 1969 .Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua kila nchi ina utaratibu wake wa ndani wa kisheria wa kushughulikia mambo yake ya ndani lakini sheria hizo hazipaswi kukiuka huo wa haki za binadamu ikiwa ni pamoja na haki za wafungwa.

**Mheshimiwa Spika,** Watanzania waliofungwa nchini China wamekuwa wakipata mateso makubwa sana ambayo ni kinyume kabisa na haki za binadamu na udhalilishaji mkubwa wa utu wa mwanadamu. Mpaka sasa Watanzania waliofungwa nchini China katika magereza mbalimbali wanakadiriwa kuwa takribani wafungwa 330.

**Mheshimiwa Spika**, Magereza yaliyoyalalamikiwa kwa ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu ni pamoja na YINGDE PRISON - GUANZIHOU WANDONG PROVINCE RPRC. (People republic of China) ambalo lina umbali wa karibu kilometer 180 kutoka Kaskazini mwa mji wa Gucughazou. Gereza hili linawafungwa takribani elfu nane wengi wao wakiwa ni mataifa kutoka Afrika.

**Mheshimiwa Spika**, Wafungwa hao wamelalamika kufungwa kwa muda mrefu na baadae wanatumika kama watumwa. Katika magereza hayo kifungo kikubwa huwa sio zaidi ya miaka sita lakini wengi hufungwa mpaka miaka thelathini ili tuu kupata nguvu kazi ya shughuli mbalimbali za kizalishaji. Sababu kubwa zinazotolewa ni kukosekana kwa wasimamizi wa kisheria kwa Watanzania hao. Mfano wa

*baadhi* ya Watanzania waliofungwa muda mrefu katika gereza la YINGDE ni pamoja na Rajab Salim Mwanyenza na Mohamed Bakari Mkemi.

**Mheshimiwa Spika,** ni ukweli kwamba nchi nyingi za Mashariki ya Mbali, hutetewa na sheria zao pale ambao panatokea kutofautiana kati yao na watu wa Mataifa mengine. Hivyo Wazawa za nchi hizo wana haki zaidi mbele ya vyombo vya dola kuliko watu wa mataifa mengine.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kuwa inawezekana kabisa Watanzania hao wamejikuta katika magereza hayo kwa sababu mbalimbali lakini ni muhimu kama nchi kuonyesha kuwa pamoja na makosa yao inathamini uraia wao.Wajibu mkubwa wa Serikali ni kuhakikisha haki na usalama wa raia wake inakuwa ni kipaumbele cha kwanza. Pamoja na Serikali kuwatambua kuwa wako magerezeni ni kuwatembelea, kuwasikiliza na kuhakikisha kuwa adhabu zao zinatekelezwa kama zilivyotakiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa inafuatilia kwa karibu hukumu zinazohusiana na Watanzania walio kwenye mataifa wanayoiwakilisha nchi yetu na pia kutoa tamko pale inapobidi kwa nia njema ya kutetea haki za raia wake nje ya nchi.

## 11.0 JINA LA MWALIMU NYERERE NA HISTORIA INAYOPASWA KUENDELEZWA

**Mheshimiwa Spika,** ni takribani miaka 18 sasa tangu Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alipotangulia mbele za haki. Pamoja na kuwa Mwalimu hayupo nasi kimwili bado tunatambua mawazo yake na mchango wake mkubwa hasa katika kupigania uhuru wa bara la Afrika na mchango mkubwa wa kisiasa katika nchi za Kikomunist.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaungana na wadau wengine mbalimbali ambao wameendelea kumuenzi Mwalimu na kutambua mchango wake. Tutakumbuka mchango mkubwa wa Mwalimu hasa katika elimu na uandishi wa vitabu. Mwalimu aliwahi kutafsiri vitabu vya Mashairi vilivyoandikwa na Shakespear ikiwemo kitabu kilichoitwa "***Julius Caesar"*** and kingine ni ***"The Marchant of venice".***

**Mheshimiwa Spika,**huu ni mchango mkubwa wa Mwalimu katika kukuza lugha ya Kiswahili ulimwenguni.Pamoja na hilo Mwalimu ameandika vitabu na Machapisho mbalimbali yakiwemo Ujamaa -essays on socialism. Uhuru na Umoja (Freedom and unity), Crusade of liberation, Man and development, Freedom and development, Women freedom: Women are eagles not chickens, Uongozi na hatma ya Tanzania, Tujisahihishe, Freedom and a new world economic order n.k.

**Mheshimiwa Spika,** kwa sasa tunashida kubwa katika masuala ya kiuongozi. Kutokana na matatizo hayo Tanzania inaanza kukosa uhalali wa kuwa nchi ambayo ni mfano

bora kwa mataifa mengine barani Afrika kama ilivyokuwa kwa utawala wa Mwalimu Nyerere. Rejea mbalimbali za kauli za Mwalimu Nyerere zimeanza kuwa mwiba kwa baadhi ya viongozi wa umma.

**Mheshimiwa Spika,** katika kitabu maarufu cha Uongozi na hatma ya Tanzania kilichopigwa marufuku kuchapishwa hapa nchini baada ya Mwalimu Nyerere kustaafu, mpaka pale alipoamua kuchapisha kitabu hicho nchini Zimbabwe ni ushahidi tosha kwamba tulianza kupanda mbegu ya kuporomosha misingi ya utawala bora na kupoteza mvuto kwa mataifa mengine.

**Mheshimiwa Spika**, zaidi ya nusu ya machapisho ya Mwalimu aliyoyaandika baada ya kustaafu yalijikita katika masuala ya uhuru na haki kwa raia, uongozi bora na misimamo mbalimbali ya taifa hili dhidi ya mataifa mengine. Kwa sasa mambo haya yote yamepigwa teke. Na ndio maana wananchi wetu wanateseka, kubaguliwa na hata kuuawa katika mataifa mengine lakini Serikali ya sasa imekaa kimya kabisa na haina namna ya kujipambanua kusimamia haki wala kuizingumzia demokrasia nje ya mipaka yetu

**Mheshimiwa Spika,** Kambi rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuchukua hatua za makusudi katika kutengeneza tovuti maalum kwa hifadhi ya kumbukumbu za Mwalimu Nyerere tofauti na ilivyo sasa ambapo kazi kubwa ya kuendeleza jina la Hayati Baba wa Taifa katika medani za Kimataifa inayofanywa zaidi na taasisi binafsi. Badala ya Serikali

kudhani kuendelea kutumia majina ya Mwalimu Nyerere kwenye majengo na barabara ndio njia pekee katika kuenzi basi ni vyema sasa Serikali ichukue wajibu wa kutengeneza tovuti maalumu kwa ajili ya maarifa na urithi wa elimu aliyotuachia katika kumuenzi na kuyaishi yale aliyoacha hasa katika kutafakari manufaa ya mahusiano baina ya nchi yetu na mataifa mengine.

## 12.0 KUKAMATWA KWA MAGARI YA MIZIGO YANAYOFANYA BIASHARA KATI YA TANZANIA, ZAMBIA NA CONGO

**Mheshimiwa Spika,** kwa takribani miezi mitatu sasa magari zaidi ya 500 yenye namba za usajili kutoka Tanzania yamekamatwa nchini Zambia na mpakani mwa Congo kwa madai kuwa magari hayo yanafanya biashara kwa njia ambazo sio halali. Magari haya yamekamatwa katika maeneo ya Nakonde, Mkushi na Kasumbalesa.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na madai hayo yaliyotolewa na Serikali ya Zambia kwa wafanyabishara kutoka Tanzania ambao walikuwa wakisafirisha mizigo hiyo kutoka Bandari ya Dar es Salaam kwenda nchini Congo, wafanyabiashara hao waliwasilisha nyaraka mbalimbali za kufanya biashara pamoja na zile za kutimiza masharti yaani (movement sheets na nyingine)na zikafanyiwa ukaguzi lakini mpaka leo magari na mizigo yao inashikiliwa.

**Mheshimiwa Spika,** wafanyabiashara hawa walichukua hatua zaidi ya kupeleka malalamiko yao ubalozini lakini jitihada hizo hazikuzaa matunda kwa kuwa ubalozi wa Tanzania nchini Zambia haujapewa ushirikiano wowote

kutoka ndani ya Serikali ya Zambia**.** Mpaka sasa hata ubalozi wa Zambia nchini haujatoa mrejesho wowote hata baada ya kufikishiwa suala hili.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na magari haya kushikiliwa yakiwa na mzigo mpaka sasa Wafanyabiashara hao wamepata hasara ya takribani dola 5,000,000 kwani kwa safari moja tu ya nchini ni dola 10,000.Hivyo wafanyabiashaa hawa wamekosa safari za kwenda na kurudi na hivyo kupoteza fedha nyingi na Serikali kukosa kodi. Serikali itambue kuwa kwa kadiri magari hayo yanavyozidi kukaa katika ardhi ya Zambia faini inazidi kujilimbikiza kwani kwa siku inagharimu dola 40 mpaka 90. Familia nyingi nchini ziko katika wakati mgumu kwani madereva wa malori hayo wapatao 500 na wasaidizi wao 500 wako katika hali ngumu kiuchumi kwani hutegemea kazi hii ya kusafirisha mizigo ili wapate kipato.Pamoja na hayo maisha ya madereva hawa yapo hatarini kw kuwa wanalazimika kulala nje ili kulinda mizigo yao.

**Mheshimiwa Spika**, tatizo hili linajulikana kwani Mheshimiwa Waziri alitoa ahadi ya kulifikisha kwa Mheshimiwa Rais. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua yafuatayo:

- Je, Mheshimiwa Rais alichukua hatua gani baada ya kufikishiwa habari hii na Mheshimiwa Waziri ikiwa tatizo hili limedumu kwa takribani miezi mitatu sasa
- Je, hali ya mahusiano kati ya Tanzania na Zambia yakoje kwa sasa?Hii ni kutokana na hali ya sintofahau

ya Serikali ya Zambia kushikilia magari haya bila kutoa kauli yoyote

- Je, Serikali inatoa kauli gani pale ambapo ubalozi wa nchi nyingine ndani ya nchi yetu wanaombwa msaada lakini hawatoi ushirikiano au pale ambapo ubalozi wa nchi yetu ndani ya ardhi ya nchi nyingine kunyimwa ushirikiano hasa katika masuala muhimu ya kulinda haki, heshima na utu wa raia yake.

## 13.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** kambi ya upinzani inaamini kuwa iwapo Wizara hii na Serikali hii kwa pamoja wataacha ujuaji na kuamua kuufanyia kazi ushauri tulioutoa; Watafikiri tofauti, kupanga tofauti na hatimaye kutenda tofauti; Na ikiwa kila mtumishi wa Wizara hii ataachana na utendaji wa mazoea wa Serikali za CCM (business as usual);

Basi Tanzania, kwa mara ya kwanza, tutashuhudia Tanzania iliyo tofauti, yenye kupiga kasi kubwa ya kimaendeleo ambayo haijapata kutokea ndani ya historia ya uhai wa Taifa hili.

**Mungu ibariki Afrika, Mungu ibariki Tanzania,**

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha.

Mchungaji Peter Simon Msigwa (Mbunge)

**Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Wizara ya**

# Mamboya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.
# 29/05/2017